

HALMASHAURI YA WILAYA YA MBULU

MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA KATIKA UKUMBI WA HALMASHAURI TAREHE 08.11.2021

MAHUDHURIO

1. Moses Nduligu	Mwenyekiti
2. Faustine Safari	Katibu
3. Finias Kagenda	Mjumbe
4. Horace Kolimba	Mjumbe
5. Gwandumi Mwambage	Mwanasheria

MUHT NA: 01/11/2021-2022: KUFUNGUA KIKAO

Mwenyekiti alifungua kikao mnamo saa tisa (9:00) kamili alasiri kwa kuwakaribisha wajumbe wote katika kikao cha siku hiyo.

MUHT NA: 02/11/2021-2022: KUSOMA NA KUTHIBITISHA AGENDA ZA KIKAO

Agenda za kikao ziliwasilishwa. Wajumbe walizipokea na kutibitisha kuwa ni agenda za kikao cha siku hiyo. Agenda zilikuwa kama ifuatavyo:

- 1) Kufungua kikao
- 2) Kusoma na kuthibitisha agenda za kikao
- 3) Taarifa ya mapokezi ya fedha shilingi za Kitanzania 950,000,000.00 kwa ajili ya miradi mbalimbali
- 4) Kupokea na kupitisha taarifa ya manunuzi yaliyofanyika pasipo kufanyika kwa kikao cha Bodi ya Zabuni "Circular Resolution"
- 5) Mengineyo kwa idhini ya mwenyekiti
- 6) Kufunga kikao

MUHT NA: 03/11/2021-2022: TAARIFA YA MAPOKEZI YA FEDHA SHILINGI ZA KITANZANIA 950,000,000.00 KWA AJILI YA MIRADI MBALIMBALI

Katibu aliwaeleza wajumbe kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu imepokea kiasi cha fedha shilingi 950,000,000.00 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi kama ifuatavyo;

- Ujenzi wa madarasa-mradi wa uviko-19 =780,000,000.00
- Ujenzi wa madarasa 4 ya shule shikizi mbili =80,000,000.00
- Ujenzi wa nyumba ya mtumishi wa idara ya afya-mradi wa uviko -19 =90,000,000.00

Katibu aliwaeleza kuwa fedha za miradi ya uviko pamoja na zile za ujenzi wa shule shikizi zimekuja na maelekezo kuwa ujenzi huo utumie utaratibu wa Force Account katika utekelezaji wake.

Wajumbe walipitia taarifa iliyowasilishwa na kujadili.

Wajumbe walikubaliana na maelekezo kuwa utaratibu wa Force Account utumike katika kutekeleza miradi hiyo. Aidha walisisitiza Kitengo cha Ununuzi kushirikiana kwa ukaribu na watekelezaji wa miradi hiyo ambao hawana utaalamu wa manunuzi.


MUHT NA: 04/05/2021-2022: MENGINEYO KWA IDHINI YA MWENYEKITI

Hapakuwa na mengineyo

MUHT NA: 07/05/2021-2022: KUFUNGA KIKAO


Mwenyekiti alifunga kikao mnamo saa 10:50 jioni akiwashukuru wajumbe kushiriki kikamilifu katika kikao hicho

UMETHIBITISHWA



Moses Nduligu

MWENYEKITI



Faustine Safari

KATIBU

TAREHE